# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU

**SHULE YA SEKONDARI MAGU,**
**S.L.P 186,**
**MAGU.**
**01/06/2024.**

**MAWASILIANO:**
**MKUU WA SHULE:** ***0765 620 813***
**MAKAMU MKUU WA SHULE:** ***0758256423/0769740853***
**MATRON/PATRON:** ***0754305499/0622870435***
**MTAALUMA:** ***0756491309***
***Email; maguseconday@yahoo.com***

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**
**……………………………………………………….**
**S.L.P ……………………………………………..**
**……………………………………………………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MAGU HALMASHAURI YA MAGU MKOA WA MWANZA MWAKA 2024.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2024/2025 tahasusi ya ______________________. Shule ya Sekondari Magu ipo umbali wa Km 2 magharibi mwa mji wa Magu. Usafiri wa mabasi kutoka mwanza mjini unapatikana katika kituo cha mabasi cha nyamhongolo nauli ni Tsh. 3000/=. Kwa wanaotoka Musoma, shuka stend ya mabasi ya magu panda usafiri wa Pikipiki kwa nauli ya Tsh. 1000/= hadi shuleni.

   Muhula wa masomo utaanza pale tarehe na mwezi husika itakayotangazwa na wizara. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe itakayotangazwa na wizara.

   **Zingatia:**
   Vifaa vyote vinavyotumia umeme haviruhusiwi shuleni. Kama **vile Radio, Pasi, Simu, Hita Ipod, Earphone n.k**. Akipatikana mwanafunzi yeyote anayetumia au kumiliki vifaa hivyo atafukuzwa shule mara moja kwa mujibu wa sheria na taratibu za shule.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia**

**2.1 Sare ya shule:-**

**a) Sare ya Shule hii ni:**

**i.** Shati mbili za kitambaa cha **TETRON,** rangi nyeupe, mikono mirefu na ambazo hazibani mwili na ziwe na mfuko mmoja tu kushoto (zitavaliwa kwa kuchomekewa). Pia, ziwe na doti moja size ya shilingi mia upande wa bega la kushoto, rangi ya dark blue kwa kidato cha tano.

**ii. Kwa wavulana**
Suruali mbili rangi ya **DARK BLUE** zenye malinda mawili ya cross pembeni, mfuko mmoja nyuma upande wa kulia na upana chini ya miguu iwe inchi 17 na iwe na turn up. (**isiwe modo)** na ifike kwenye kifundo cha miguu (kwa atakayehitaji atashonewa shuleni)

**iii. Kwa wasichana**
Sketi mbili za rangi ya ***DARK BLUE*** upana wa malinda ya sketi uwe kati ya Inchi 1 ½ na 2 zenye **belt** ndogo. **(Belt pana haikubaliki**) urefu kwenda chini iguse kifundo cha miguu au sentimeta 10 kutoka kwenye unyayo wa miguu. Hairuhusiwi kuwa na mikanda nyuma.

**iv.** Kwa wasichana wa kiislam wanaweza kushona blauzi ya mikono mirefu rangi nyeupe mbili na kijuba rangi nyeupe mbili. (kwa atakayehitaji atashonewa shuleni)

**b)** Sare ya michezo ni jezi rangi **BLUE** na track suit rangi **BLUE**(pembeni iwe na mistari myeupe na isiwe na maandishi yoyote)zenye nembo(.Kwa anehitaji pia inapatikana shuleni)

**c)** Viatu vya shule ni vya ngozi rangi nyeusi vyenye kisigino kifupi, vya kufunga gidamu yaani kamba. (Boots na raba nyeusi haziruhusiwi)

**d)** Soksi jozi mbili nyeupe zisizo na mapambo yoyote wala maandishi.

**e)** Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali kwa wavulana.

**f)** Tai mbili za blue yenye michirizi myeupe zenye nembo(Punda milia), (kwa atakayehitaji Zinapatikana shuleni).

**g)** Raba za michezo rangi yoyote.

**2.2 Michango mbalimbali ya shule.**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Maelezo muhimu**:-**

**a)** Fedha ya michango yote ***ilipwe kwenye akaunti ya shule No. 31201200067 (Jina la Akaunti ni Magu Secondary School recurrent Account, Bank ya NMB)***

- **Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye Bank pay in slip.**

**b) Mahitaji mbalimbali yanayohitajika.**

**1. Mahitaji muhimu anayopaswa kuleta shuleni.**

- **i)** Ream mbili (02) za karatasi (**Double A mbili (2)**
- **ii)** Ndoo mbili (ndogo moja lt10 na kubwa moja lt20) zenye mifuniko
- **iii) Vifaa vya usafi:-**

Wanafunzi wa tahasusi zote wanatakiwa kuleta vifaa vya usafi vifuatavyo:-

HKL

- Kwanja 1
- Panga(kwa ajili ya kuproon miti na matengenezo ya mazingira)1

CBG

- Jembe na mpini 1
- leki 1

PCB

- Kwanja 1
- Mfagio mlaini kufagia ndani (soft broom) 1

PCM

- Mfagio mgumu wa kusugulia masinki (hard broom) 1
- Squeezer(mopa) 1

PGM

- Jembe na mpini 1
- Mfagio mlaini (soft broom)

***N.B. Tracksuit tai, tishet, na sweta (VYENYE NEMBO)Vinapatikana shuleni hivyo unashauriwa kama vitu hivyo ni vigumu kuvipata katika mazingira uliopo waweza kuja kununulia maeneo haya.***

**2. Mahitaji muhimu anayopaswa kuwa nayo mwanafunzi awapo shuleni.**

- **i.** Rim moja (01) (***Ruled paper*** kwa ajili ya mazoezi ya darasani)
- **ii.** Unashauriwa kuja na vitabu vya ziada kwa ajili ya kujisomea(orodha imeambatanishwa)
- **iii.** Dissecting kit kwa wanafunzi wa somo la Biology(kwa atakayehitaji zinapatikana shuleni)
- **iv.** Scientific calculator – function 991EX au 991ES kwa tahasusi za sayansi tu. (kwa atakayehitaji zinapatikana shuleni )
- **v.** Stop watch kwa wanafunzi wa tahasusi za sayansi (kwa atakayehitaji zinapatikana shuleni)
- **vi.** Godoro (Ft. 2 $\frac{1}{2}$ x 6 au 3 x 6).Godoro lazima liwe na foronya yake (cover) (kwa atakayehitaji yanapatikana jirani na shule)
- **vii.** Mashuka rangi ya bluu pair 2, foronya rangi ya bluu pair 1( kwa atakayehitaji yanapatikana shuleni)
- **viii.** Chandarua rangi ya blue 1 (kwa atakayehitaji zinapatikana shuleni)
- **ix.** Kila mwanafunzi anapaswa kuja na taa ya solata itatumika pale umeme unapokatika. (lazima)
- **x.** Blanketi 1 kwa wale tu wenye matatizo ya kiafya.
- **xi.** Kila mwanafunzi anapaswa aje na BIMA ya afya ya NHIF kama hana aje na shilingi 50400/= kwa ajili ya kutengenezewa BIMA ya NHIF kwa ajili ya matibabu yake.Ilipwe kwenye A/C 31202500187 Elimu ya kujitegemea magu day (kwa mwaka).
- **xii.** Vyombo vya chakula:- sahani, bakuli, kijiko na kikombe.
- **xiii.** T-shirt rangi orange halisi yenye nembo ya shule (kwa atakayehitaji zinapatikana shuleni),kwa wasichana waislam ni pamoja na kijuba rangi ya orange
- **xiv.** Sweta rangi ya blue moja yenye nembo ya shule (kwa atakayehitaji zinapatikana shuleni)

**xv.** Sanduku kubwa la chuma(Tranka)

**xvi.** Nguo za kushindia (shamba dress) ni:-

**a)** **Wasichana –** Gauni **kitambaa cha draft** (vizano) za rangi nyekundu , dark blue na nyeupe mshono wa solo ndefu, isiyobana mikono mifupi. Vilevile, mikono mirefu kijuba kiwe cha rangi nyeusi kwa wasichana wa kiislam. Kitambaa kiwe kizito (jozi 2) (kwa atakayehitaji zinapatikana shuleni

**b)** **Wavulana suruali** nyeusi zenye malinda mawili ya cross pembeni, mfuko mmoja nyuma upande wa kulia na upana chini ya miguu iwe inchi 17 na iwe na turn up. (**isiwe modo)**. (kwa atakayehitaji zinapatikana shuleni)

**c)** Mwanafunzi aje amevaa sare ya shule pindi anaporipoti shuleni, *nguo za nyumbani haziruhusiwi **kabisa.***

**d)** Mwanafunzi aje na spring file 2.

**e)** Wanafunzi wa tahasusi za sayansi yaani PCB, PCM ,PGM na CBG waje na lab coat rangi ya nyeupe kwa atakayehitaji zinapatikana shuleni)

**MUHIMU:**

Mafuta ya kubadilisha rangi ya ngozi, mafuta yenye harufu kali (perfum, body spray, poda, wanja, lipstic pamoja na make up), nywele zilizowekwa dawa, piko, wave, zilizosukwa, kucha zenye rangi na hina, hereni, pete, cheni na urembo wa aina yoyote (**HAVIRUHUSIWI SHULENI).**

## SHERIA ZA SHULE.

1. Mwanafunzi lazima awe na hekima, utii kwa walimu, viongozi, watu wazima, wageni na kati yao wenyewe.
2. Ni wajibu wa mwanafunzi kutunza mali za shule.
3. Wanafunzi hawaruhusiwi kuvuta sigara, kunywa pombe, kunywa vidonge vya kulevya au kuvuta bangi pamoja na wizi.
4. Wanafunzi hawaruhusiwi kufika nyumbani kwa walimu bila ruhusa na nje ya mipaka ya shule wakati wa masomo.
5. Ni marufuku kuingia nyumba za starehe kama vile baa ya pombe, dansini, na nyumba za kulala wageni (Guest House).
6. Ni wajibu wa wanafunzi kuona kuwa viwanja vya shule, madarasa na vyumba vingine vimewekwa katika hali ya usafi.
7. Matusi ya kusema au kuandika na ugomvi ni marufuku.
8. Mwanafunzi lazima ahudhurie vipindi vya dini yake kila siku.
9. Ni mwiko kwa wanafunzi kujiunga na vikundi vyenye tabia mbaya shuleni au nje ya shule.
10. Kila mwanafunzi anapaswa kuhesabu namba saa 1:00 asubuhi na kuwahi paredi saa 1:30 asubuhi kuhudhuria vipindi vyote vya masomo na kufanya kazi zote anazopewa na mwalimu.
11. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kushiriki kikamilifu katika mipango yote ya shule ya Elimu ya kujitegemea. Uvivu au utoro ni makosa makubwa.
12. Ni marufuku kupokea wageni. Wageni wapitie kwa mkuu wa shule.
13. Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka nje ya shule mara waingiapo bila ruhusa ya uongozi wa shule.
14. Ni marufuku kuzagaa kwenye baraza la shule au nje ya madarasa wakati wa vipindi.
15. Mwanafunzi haruhusiwi kujipikia au kuchemsha chochote awapo shuleni, pia pasi za mkaa na umeme haziruhusiwi kabisa.
16. Ni marufuku kujiunganishia au kuunganisha umeme katika maeneo yote ya shule.
17. Mwanafuzi haruhusiwi kuvaa nguo ambazo sio sare ya Shule (nyumbani) pamoja na viatu ambavyo si sare ya shule ndani na nje ya Shule.
18. Ni marufuku kuonekana, kulala bwenini wakati vipindi vinaendelea darasani.
19. Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu au kutumia simu katika mazingira ya shule au nje ya shule bila ya mwalimu.

**20.** Matumizi ya simu au mawasiliano kwa wazazi yapitie ofisi ya makamu mkuu wa shule

## UTARATIBU UNAOPASWA KUFUATWA NA MWANAFUNZI ANAPOKUWA SHULENI.

1. Kuhudhuria roll call kila saa 11:30 jioni.
2. Atawajibika kutunza mali na vifaa mahali anapoishi. Uharibifu ukitokea utawajibika.
3. Kushiriki mchaka mchaka saa 12:00 – 12:30 Asubuhi.
4. Kuhudhuria muda wa maandalizi binafsi darasani (preparation time) saa 2:00 usiku – 5:00 usiku.
5. Atapaswa kuwa bwenini baada ya “preparation time”.
6. Wanafunzi wawapo bwenini baada ya “preparation time” taa zitazimwa.
7. Mwanafunzi awapo shuleni na hata kama ataomba ruhusa kwenda nje ya maeneo ya shule atapaswa kuvaa sare ya shule muda wote. Hivyo anaruhusiwa kushona sare ya ziada.
8. Kufanya mitihani yote ya nje na ndani ya shule ni lazima, mwanafunzi atakayekwepa kwa makusudi kufanya mtihani atatungiwa mtihani mwingine na kulipia gharama za mtihani huo.
9. Mwanafunzi wa bweni haruhusiwi kutumia, kumiliki au kukutwa na simu ndani au nje ya eneo la shule.

## MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

- **i)** Wizi.
- **ii)** Kugoma na kuhamasisha mgomo.
- **iii)** Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
- **iv)** Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
- **v)** Kusuka nywele kwa mtindo usio kubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
- **vi)** Kufuga ndevu.
- **vii)** Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
- **viii)** Uvutaji wa sigara.
- **ix)** Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
- **x)** Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
- **xi)** Kupata ujauzito au kutoa mimba.
- **xii)** Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
- **xiii)** Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
- **xiv)** Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
- **xv)** Kudharau Bendera ya Taifa
- **xvi)** Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
- **xvii)** Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.
- **xviii)** Kupunguza suruali tofauti na vipimo vya shule (modo)

## VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU.

- **a)** Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.
- **b)** Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
- **c)** Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanunni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**d)** Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

**e)** Mwanafunzi aje na result slip na cheti cha kuzaliwa.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBUNI SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAGU**

**HERI R. NZIGO**
**MKUU WA SHULE**

THE HEADMASTER
MAGU SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 186
MAGU

**FOMU NA PICHA ZA WAZAZI NA NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI WANAOWEZA KUMTEMBELEA MWANAFUNZI SHULENI PAMOJA NA NAMBA ZAO ZA SIMU.**

| NA. | JINA LA NDUGU | MAHUSIANO | NA. YA SIMU | PICHA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ____________________ | ______________ | ______________ | |
| 2. | ____________________ | ______________ | ______________ | |
| 3. | ____________________ | ______________ | ______________ | |
| 4. | ____________________ | ______________ | ______________ | |

**FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI, KULIPA ADA, MICHANGO NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE.**

Mimi ____________________________________________ (Jina la mwanafunzi) nimesoma, nimeelewa na ninakubaliana na maagizo yote yanayoelekezwa katika barua ya maelezo niliyopewa na shule hii. Ninaahidi kwamba nitafuata sheria zote za shule na kutimiza wajibu wangu katika muda wote nitakapokuwa mwanafunzi wa shule hii.

Sitajihusisha na mgomo wala kuchochea mgomo, makosa ya jinai au kujihusisha na vitendo vinavyohatarisha amani ya shule hii. Kwa jinsi hiyo uongozi wa shule uchukue hatua ya kuniondoa au kunisimamisha masomo au adhabu yoyote pale nitakapokwenda kinyume na maagizo, kanuni na sheria za shule. Ninaahidi pia kuwa nitajielimisha kwa kadri ya uwezo wangu.

Sahihi ya Mwanafunzi ………………………………………………..
Jina la mwanafunzi …………………………………………………….
Tarehe ……………………………………………………………………
Sahihi ya Mzazi / Mlezi ……………………………………………….
Jina la Mzazi / Mlezi ………………………………………………….
Namba ya simu ………………………………………………………..
Tarehe …………………………………………………………

# UNASHAURIWA KUJA NA VITABU VYA ZIADA ANGALAU VIWILI KWA KILA SOMO KULINGANA NA TAHASUSI UNAYOSOMA.

## BIOLOGY

**A.** Comprehensive Biology.
**B.** Biological Science.
**C.** Understanding biology.
**D.** Functional approach.
**E.** Biology form V T.I.E 2019
**F.** Biology form VI T.I.E 2019
**G.** Raven Johnson Biology 8th Edition
**H.** CHAND.

**CHEMISTRY:**

**A.** Conceptual Chemistry Chand XI, XII
**B.** A-level chemistry ramsden 4th Edition.
**C.** Organic Chemistry part 1, 2.
**D.** ABC modern chemistry
**E.** Chemistry TIE

**PHYSICS:**

**A.** Principles of physics. By Nellcon.
**B.** Principles of physics by Chand.
Class XI and XII) **– NI LAZIMA**
**C.** Roger Muncaster.
**D.** ABC Modern Physics 1, 2

**KISWAHILI**

**USHAIRI**

**A**. Fungate ya uhuru
**B**. Chungu tamu
**C**.Kimbunga

**RIWAYA**

**A**.Vuta nkuvute
**B**. Mfadhiri
**C**. Usiku utakapoisha

**TAMTHILIYA**

**A**.Moran
**B**.Nguzo mama
**C**. Kwenye ukingo wa thimu

**ADVANCED MATHEMATICS**

**A.** Chand class XI
**B.** Chand class XII vol. 1
**C.** Chand class XII vol. 2 **(Lazima)**
**D.** Pure mathematics one by Back house.
**E.** Pure mathematics two by back house
**F.** Advanced mathematics by Tranter
**G**. Advanced mathematics form V & VI TIE

**GEOGRAPHY**

**A.** An Integrated Regional Study on Human and Economic Geography.
**B.** Africa In Diagram **–** By Bunnet
**C**. Physical Geography TIE
**D**. Human and Economic Geography TIE
**E**. Practical Geography TIE

**HISTORY**

**A.** A Major Event in World History 1, 2
**B.** Mastering History 1, 2
**C.** History of Africa.

**ENGLISH**

**A**.A Man of the people
**B**.An enemy of the people
**C**.The beautiful one are not yet born
**D**.Theory of literature ADVANCED LEVEL

## TAARIFA MUHIMU KWA MWANAFUNZI.

**1.** Jina lako ………………………………………………… ( jina hili ni lazima lifanane na jina ulilokuwa unatumia kidato cha nne )

**2. BABA:**

i) Jina la baba yako …………………………………………………….
ii) Yu – Hai ……………………………………………………………..
iii) Kama amefariki taja ni lini ………………………………………………….
iv) Anuani yake ……………………………….. (namba za simu) …………………..
v) Kazi na cheo chake …………………………………………………….
vi) Dini ya baba yako ……………………………………………………

**3. MAMA:**

i) Jina la mama yako …………………………………………………….
ii) Yu – Hai ……………………………………………………………..
iii) Kama amefariki taja ni lini ………………………………………………….
iv) Anuani yake ……………………………….. (namba za simu) …………………..
v) Kazi na cheo chake …………………………………………………….
vi) Dini ya mama yako ……………………………………………………

**4. MLEZI.**

(i). Unaye mlezi? ( mlezi ni mtu asiye mzazi wako) anayekutunza na kukuhudumia kwa chakula, malazi n.k

(ii). Ndiyo/ Hapana……………………………………………………………….

**a)** Jina la mlezi huyu ni ……………………………………………………..

**b)** Uhusiano wako na mlezi ( mjomba, kaka, rafiki, shangazi n.k) …………………………

**c)** Anuani ya mlezi wako ni ……………………………………………………..

**d)** Kazi ya mlezi wako ni ……………………………………………………..

**5.** i) Jina la mtu anayepelekewa ripoti zako za shule kama si baba au mama au mlezi wako ni nani?
…………………………………………………………………………….
Anuani yake ni …………………………………………….
Sahihi ya Mwanafunzi …………………………………….

Tafadhali ambatanisha nakala ya
- Results slip ya kidato cha nne
- Cheti cha kuzaliwa.

# MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE AND TECHNOLOGY

SHULE YA SEKONDARI MAGU,
S.L.P 186,
MAGU.
**…………………………..**

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

**(To be completed by a Medical Officer)**

Pupil's full name ………………………………………………………………..

Age ………………………………………………………………………………

Blood count (Red and white) ………………………………………………………..

Stool ……………………………………………………………………………...

Urine ……………………………………………………………………………..

Syphilis Test …………………………………………………………………..

T.B.Test ………………………………………………………………………….

Eye Test …………………………………………………………………………..

Ears ……………………………………………………………………………….

Chest ……………………………………………………………………………

Spleen …………………………………………………………………………….

Abdomen ………………………………………………………………………….

**ANY ADDITIONAL INFORMATION** e.g Physical defects, Chronic or Family Diseases, etc.

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………

Signature ………………………………………………………………………..

Designation ……………………………………………………………………..

Station …………………………………………………………………………….

Date ……………………………………………………………………………….

# MFANO WA SARE ZA SHULE







**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZA SIMU ZILIZOPO KWENYE FOMU HII UKURASA WA KWANZA**